

Imetolewa tarehe: 7 Oktoba, 2010

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



TAARIFA KWA UMMA

KUONDOA AMRI YA KUSITISHA KWA MUDA UINGIZAJI, USAMBAZAJI, UUZAJI NA MATUMIZI YA MAZIWA YA NAN 2 YALIYOSAJILIWA

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii yenye jukumu la kudhibiti ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ili kulinda afya za watumiaji.

Mnamo tarehe 13 Agosti 2010, TFDA ilitoa taarifa kwa umma kuhusu kubainika kuwepo katika soko maziwa ya watoto aina ya NAN 2 ambayo ni bandia na yaliyosajiliwa na hivyo ubora na usalama wake kuwa wa mashaka.

Katika taarifa hiyo pamoja na mambo mengine, Mamlaka ilisitisha kwa muda uingizaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya maziwa ya watoto aina ya NAN 2 yaliyosajiliwa. Hatua hiyo ilifikiwa ili kuepuka mkanganyiko ambao ungeweza kujitokeza kutokana na baadhi ya watumiaji kushindwa kutofautisha maziwa ya NAN 2 yaliyosajiliwa na yale ambayo ni bandia. Mamlaka ilifanya ukaguzi na kukamata maziwa bandia ya NAN 2 na taratibu za kuyateketeza kwa mujibu wa sheria zinakamilishwa.

Kwa tangazo hili, TFDA inapenda kuutaarifu umma kuwa imeondoa amri ya kusitisha kwa muda uingizaji, usambazaji, uuzaji na matumizi ya maziwa ya NAN 2 yaliyosajiliwa ambayo yanatengenezwa na kampuni ya Nestlé ya Ufaransa. Hivyo, maziwa ya NAN 2 yaliyosajiliwa ambayo yalizuiliwa katika maeneo mbalimbali ya kuuzia vyakula wakati wa zoezi la ukaguzi, yameruhusiwa kutumika.

Hata hivyo, walaji wanashauriwa kuzingatia alama za utambuzi wa maziwa halisi ya NAN 2 yaliyosajiliwa kama ambavyo imeainishwa hapa chini;

- Mtengenezaji ni Nestlé France, SAS, F-77446, Mame la Vallee, Cedex 2, France
- Maandishi kwenye lebo yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili
- Tarakimu "2" kwenye neno NAN 2 ina rangi ya bluu
- Kwenye lebo kuna picha moja ya ndege watatu weupe ambayo ni sehemu ya nembo ya Kampuni ya Nestlé.
- Maandishi yamechapishwa kwenye kopo moja kwa moja.

Mamlaka inawakumbusha walaji kuwa waangalifu na hivyo kutumia maziwa ya watoto wachanga ambayo yamesajiliwa kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini;

Na.	Jina la maziwa	nchi yalikitengenezwa
1	Lactogen 1 Infant Formula	Ufaransa
2	Lactogen 2 Follow up Formula	Ufaransa
3	NAN 1 Starter Infant Formula	Uholanzi
4	NAN 2 Infant Formula	Ufaransa
5	Cowbell Infant Formula	Ufaransa

Imetolewa Na:

KAIMU MKURUGENZI MKUU,
MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA (TFDA),
BARABARA YA MANDELA, MABIBO - EXTERNAL,
S.L.P 77150, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 222 450512/450751/452108
Nukushi: +255 222 450793
Barua Pepe: info@tfda.or.tz; Tovuti: www.tfda